TAARIFA YA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA KWA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU WIKI NA SIKU YA SHERIA NCHINI KWA MWAKA 2023
IMETOLEWA KATIKA UKUMBI WA MAHAKAMA WA KITUO JUMUISHI CHA UTOAJI HAKI TEMEKE
TAREHE 10 JANUARI, 2023

HERI YA MWAKA MPYA 2023

Kwa niaba ya Mahakama ya Tanzania na kwa niaba yangu binafsi napenda kuwakaribisha Waandishi wa Habari katika Mkutano huu muhimu kuhusu kuadhimisha Wiki ya Sheria na SIKU YA SHERIA 2023. Awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kutujaalia sote Mwaka Mpya 2023. NAWATAKIENI NYOTE HERI YA MWAKA MPYA 2023!

WIKI YA SHERIA NA SIKU YA SHERIA 2023

Kama ilivyo kawaida, Mahakama ya Tanzania huanza mwaka wake mpya kwa kutenga wiki moja kabla kuanza shughuli za Mahakama kwa KUADHIMISHA WIKI YA SHERIA NA SIKU YA SHERIA NCHINI. Kwa mwaka huu 2023, napenda kuwataarifu kwamba maadhimisho ya wiki ya sheria yatafanyika kitaifa kuanzia tarehe

22 Januari, 2023 siku ya Jumapili hadi tarehe 29 Januari, 2023 siku ya Jumapili katika Viwanja vya *Nyerere Square* Jijini Dodoma.

MATEMBEZI KUASHIRIA KUANZA KWA WIKI YA SHERIA

Wiki ya sheria itafunguliwa kwa matembezi yatakayofanyika siku ya Jumapili tarehe 22 Januari, 2023 saa 12.00 asubuhi. Mgeni rasmi kwenye matembezi hayo anatarajiwa kuwa Mhe. Dkt. Phillip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matembezi hayo yataanzia Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki (IJC) Dodoma na yataishia kwenye Viwanja vya *Nyerere Square* Jijini Dodoma; ambapo MGENI RASMI atapata fursa ya kutembelea mabanda ya maonyesho na pia kutoa nasaha zake.

Aidha, kilele cha maadhimisho haya ni siku ya SHERIA NCHINI itakayofanyika siku ya Jumatano tarehe 01 Februari, 2023 katika viwanja vya Chinangali, Jijini Dodoma. Mgeni rasmi siku hiyo anatarajiwa kuwa MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KAULI MBIU

Kwa mwaka huu, katika maadhimisho haya ya Wiki ya Sheria na Siku ya Sheria, KAULI MBIU itakuwa: "***Umuhimu wa Utatuzi wa Migogoro kwa Njia ya Usuluhishi Katika Kukuza Uchumi Endelevu: Wajibu wa Mahakama na Wadau***."

Kauli mbiu hii imebeba ujumbe mahususi kuhusu wajibu wa Mahakama na Wadau wake katika kutumia njia ya usuluhushi kutatua migogoro kwa lengo la kukuza uchumi endelevu. Wiki ya Sheria ni wakati Mahakama, wadau na wananchi watakumbushana na kuonyeshwa athari za kesi kuchelewa kukamilika kwa uchumi wa watu na kwa uchumi wa nchi.

Ukisoma Ibara 107A(2)(d) ya Katiba, inazungumzia "kukuza na kuendeleza usuhulishi katika migogoro" Hata hivyo njia mbadala ya utatuzi wa migogoro inajumuisha utaratibu wa Usuluhishi *(Arbitration)*, upatanishi *(Mediation)*, kurudisha mahusiano ya kirafiki *(Reconciliation)* na mazungumzo kufikia makubaliano *(Negotiation)*. Katiba inaposema kuwa kauli ya mwisho ya utoaji

haki ni ya Mahakama, inatambua taasisi nyingi zinagusa masuala ya haki kabla mgogoro haujapewa kauli ya mwisho na Mahakama. Ikiwa ni lazima wasaidie suluhu.

Utatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ni takwa la Kikatiba. Njia hii ya utatuzi wa migogoro pia imehimizwa katika vitabu vya dini ambazo wengi wetu ni waumini wake. Kwa hiyo, ni mpango wa Mwenyezi Mungu kuona watu wake wanatatua tofauti zao kwa njia ya usuluhishi. Nchi yetu inazo sheria nyingi ambazo zimetoa nafasi ya usuluhishi ambazo hatuzitumii – tunakimbilia Mahakamani. Waandishi wa Habari mnayo HUDUMA YA USULUHISHI NA UPATANISHI KUTOKA BARAZA LA HABARI (MCT). Bodi ya Makandarasi ni mfano mwingine wa Taaluma zenye mifumo mizuri ya usuluhishi.

Kwa ufupi, utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi, upatanishi, kurudisha mahusiano na mazungumzo una faida nyingi ikiwa ni pamoja na:

i. Upatikanaji wa haki kwa wakati na kwa gharama nafuu;

ii. Punguza milundikano ya mashauri Mahakakani.

iii. Kuimarisha amani na ustawi wa Jamii;- Katiba yetu inasema tunajenga nchi inayozingatia misingi ya uhuru, haki na amani.

iv. Kutumia muda mfupi kushughulikia migogoro na kubaki na muda mwingi zaidi katika shughuli za uzalishaji mali na utoaji huduma;

v. Kulinda mahusiano ya wadaawa kijamii na kiuchumi;

vi. Kuhifadhi na kuendeleza mahusiano ya kibiashara na ya kijamii kwa wadaawa.

Tafiti zinaonesha kwamba Nchi nyingi zilizoendelea, usuluhishi humaliza zaidi ya asilimia 90 ya migogoro inayofikishwa mahakamani. Hali hiyo ni tofauti na nchi yetu ambapo licha ya Ibara ya 107A (2) (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi bado eneo hili halipewi kipaumbele na Wadaawa na Wadau wa Mahakama kwa ujumla. Hali hii inathibitishwa na idadi ndogo ya mashauri yanayomalizika kwa njia ya usuluhishi. Hivyo, hali hii

imeisukuma Mahakama ya Tanzania kuwa na kauli mbiu yenye lengo la kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Pia nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi wa mkoa wa Dodoma ambako maonesho ya WIKI YA SHERIA kitaifa yatafanyika wafike kwenye viwanja vya Nyerere Square ili wapate elimu mahsusi kuhusu utatuzi wa migogoro kwa njia ya usuluhishi. Lakini pia wananchi watakaofika kwenye viwanja hivyo watapata nafasi ya kutoa malalamiko, maoni na mapendekezo ya uboreshaji wa huduma za Mahakama. Ni matumaini yangu na ya Mahakama ya Tanzania, kuwa, taasisi zote zinazosimamia Sheria zinazotoa nafasi ya usuluhishi, zitumie Wiki ya Sheria kutangaza hizo fursa za usuluhishi.

Sambamba na Elimu ya Sheria na maonesho yatakayofanyika Kitaifa katika Mji Mkuu wa Tanzania, Dodoma; utoaji wa elimu ya sheria kwa umma na maonesho utaendelea pia katika Kanda za Mahakama Kuu, Mikoa na Wilaya nchi nzima kama ilivyofanyika kwa miaka mingine.

Aidha, wakati wa WIKI YA SHERIA elimu itatolewa kuhusu taratibu za ufunguaji wa mashauri hasa kwa njia ya Mtandao, Sheria na taratibu zinazotumika katika kuendesha mashauri mbalimbali kama mashauri ya Ndoa na Talaka, Ardhi, migogoro ya Kazi pamoja na utekelezaji wa hukumu, Sheria za Watoto na taratibu za mashauri ya mirathi.

Vilevile wananchi watapata fursa ya kujifunza huduma zitolewazo na Mahakama inayotembea *"Mobile Court"* na Mahakama za Vituo Jumuishi.

Wananchi watakaotembelea mabanda ya Mahakama watapata fursa ya kujifunza kwa kiasi gani Mahakama ya Tanzania imejipanga kutoa haki katika Karne ya 21 kwa kutumia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Katika maonesho hayo, elimu hiyo itatolewa na waheshimiwa Majaji, Wasajili, Naibu Wasajili, Mahakimu pamoja na Wadau wa Mahakama wakiwemo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu, Chama cha Majaji na Mahakimu Wanawake (TAWJA), Polisi, Magereza, Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) na wadau wengine.

Nitumie fursa hii kuwaomba Waandishi wa Habari kuujulisha umma wa Watanzania uwepo wa jambo hili muhimu kwa maendeleo ya sekta ya Sheria, Mahakama na uchumi wa Taifa letu. Hivyo, kupitia mkutano huu ninawaalika wananchi wote kote nchini kutembelea maonesho ya Mahakama na wadau wa sheria katika maeneo yenu mlipo ili mpate fursa ya kupata elimu kutoka kwa Wadau na Maafisa wa Mahakama watakaokuwepo katika Mabanda husika.

Mwisho, kama nilivyotangulia kueleza, rai yangu kwenu Waandishi wa Habari tumieni vyombo vyenu vya habari kuwahimiza wananchi kutenga muda wao kutembelea maonesho kote nchini ili wapate elimu juu ya umuhimu wa kutumia njia ya usuluhishi katika utatuzi wa migogoro pamoja na kujua maboresho mbalimbali ya

Mahakama yanayoendelea kupitia mpango mkakati na mpango wa maboresho unaomlenga mwanachi katika kuboresha huduma za kimahakama.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA.